### 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Matokeo ya jumla ya somo la Kiswahili katika mwaka wa 2022 yameimarika japo kwa wastani. Hata hivyo, utendaji wa asilimia kubwa ya wanafunzi ungali hafifu. Hili linadhihirika kupitia kwa matokeo ya karatasi ya tatu, ambayo japo yaliimarika (31/80), yangali mbali na alama wastani ambayo ni (40/80). Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka tisa (2014 hadi 2022 ).

**Jedwali 11**: *Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili (2014 – 2022)*

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | 1 | | 40 | 20.17 | 5.26 |
| | 2 | | 80 | 32.27 | 12.60 |
| | 3 | | 80 | 42.93 | 15.81 |
| | Jumla | 482,122 | 200 | 95.36 | 29.88 |
| 2015 | 1 | | 40 | 20.86 | 5.19 |
| | 2 | | 80 | 36.12 | 13.50 |
| | 3 | | 80 | 38.80 | 15.38 |
| | Jumla | 5211,59 | 200 | 95.76 | 31.02 |
| 2016 | 1 | | 40 | 18.23 | 5.53 |
| | 2 | | 80 | 34.11 | 13.83 |
| | 3 | | 80 | 25.67 | 12.87 |
| | Jumla | 571,176 | 200 | 77.97 | 29.07 |
| 2017 | 1 | | 40 | 18.84 | 5.23 |
| | 2 | | 80 | 25.45 | 11.79 |
| | 3 | | 80 | 25.15 | 13.42 |
| | Jumla | 610,392 | 200 | 69.43 | 27.49 |
| 2018 | 1 | | 40 | 16.98 | 4.82 |
| | 2 | | 80 | 27.22 | 10.88 |
| | 3 | | 80 | 22.20 | 11.95 |
| | Jumla | 659,465 | 200 | 66.40 | 24.76 |
| 2019 | 1 | | 40 | 19.88 | 5.43 |
| | 2 | | 80 | 36.50 | 12.64 |
| | 3 | | 80 | 21.08 | 12.64 |
| | Jumla | 694,982 | 200 | 77.46 | 28.03 |
| 2020 | 1 | | 40 | 20.19 | 5.28 |
| | 2 | | 80 | 34.99 | 12.81 |
| | 3 | | 80 | 25.88 | 16.00 |
| | Jumla | 743,395 | 200 | 81.05 | 31.28 |
| 2021 | 1 | | 40 | 19.44 | 6.28 |
| | 2 | | 80 | 31.46 | 12.93 |
| | 3 | | 80 | 31.19 | 19.48 |
| | Jumla | 822,267 | 200 | 82.09 | 35.34 |
| 2022 | 1 | | 40 | 19.70 | 5.69 |
| | 2 | | 80 | 35.73 | 12.45 |
| | 3 | | 80 | 31.21 | 17.42 |
| | Jumla | 876,916 | 200 | 86.64 | 32.15 |



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

(i) Utendaji wa watahiniwa katika utungaji umeimarika japo kwa kiwango hafifu. Haya yanadhihirishwa na kupanda kwa nukta chache mno kwa alama wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) kutoka **19.44** mwaka 2021 hadi **19.70** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **37/40** ikilinganishwa na **39/40** ya mwaka jana. Ni watahiniwa **wanne** tu ambao walipata alama hii. Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi ni **22/40**. Jumla ya watahiniwa waliotuzwa alama hii ni **60,609.** Kutokana na uchanganuzi, ni dhahiri kwamba idadi ya watahiniwa ambao walipata asilimia sabini **(28/40)** ilishuka kiasi kutoka **27,586 (3.33%)** mwaka 2021 hadi **23,475 (2.66%)** mwaka huu. Asilimia ya watahiniwa waliopata alama za chini zaidi iliongezeka. Kwa mfano, idadi ya watahiniwa waliopata alama 1/40 ilipanda kutoka **817** mwaka wa 2021 hadi **1,532** mwaka huu.

(ii) Hata hivyo, uchanganuzi umedhihirisha kwamba bado kuna wanafunzi ambao wana changamoto kubwa katika kujieleza. Haya yananadhihrishwa na, kwa mfano, watahiniwa **6,188** ambao walipata alama **5/40**. Imebainika kwamba wanafunzi **13,793** walipata baina ya alama **1** na **5.** Hali hii ni ya kutia wasiwasi ikilinganishwa na mwaka wa 2021 ambapo watahiniwa **7,688** walikuwa katika safu hii. Pia, karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(5.69)** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida **(15.00).** Hali hii inaweza kuhusishwa na watahini kuwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

(iii) Alama ya wastani ya karatasi ya pili **(102/2)** imeimarika kwa pointi **4.27** kutoka **31.46** mwaka 2021 hadi **35.73** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa mwaka 2022 ni **80/80** ikilinganishwa na **75/80** ya mwaka 2021. Ni mwanafunzi **mmoja** tu ambaye alipata alama hii. Idadi wa tatahiniwa waliopata baina ya **70/80** na **80/80** ilishuka kwa kiwango kikubwa kutoka **371** mwaka 2021 hadi **131** mwaka huu. Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi **(25,829)** ni **36/80.** Hali kadhalika, imebainika kwamba idadi ya watahiniwa wanaopata alama za juu ilishuka kwa kiwango kikubwa. Mathalan, idadi ya wanafunzi waliopata asilimia **70 (56/80)** katika karatasi hii iliimarika kutoka **5,406** mwaka 2021 hadi **9,197** mwaka 2022. Karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ilishuka kiasi kutoka **12.93** ya mwaka 2021 hadi **12.45** mwaka huu.

(iv) Uchanganuzi umebainisha kwamba bado kuna wanafunzi ambao umilisi wao ni wa kiwango cha chini. Idadi muhimu ya watahiniwa ilipata alama za chini. Kwa mfano, wanafunzi **4,324** walipata baina ya alama **1/80** na alama **5/80** ikilinganishwa na watahiniwa **6,384,** waliokuwa katika kitengo hiki mwaka 2021. Hali kadhalika, ruwaza za matokeo zinaonyesha kuwa matokeo ya karatasi hii yamekuwa yakiyumba tangu mwaka wa 2009. Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi (10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta tatu sufuri (14.30)** mwaka 2012. Mwaka 2013 ilipanda kwa kiasi kidogo mno, mwaka 2014 kwa **2.35,** na mwaka 2015 kwa takriban alama **4**. Mwaka 2016 alama ilishuka kwa takriban alama **2,** Mwaka 2017 alama hii ilishuka kwa zaidi ya alama **8**. Mwaka 2018 alama wastani ilipanda kwa takriban alama **2**, mwaka wa 2019 ilipanda kwa alama **9.28,** mwaka wa 2020 na 2021 ilishuka kwa kwa alama **1.51** na **3.53** mtawalia. Mwaka wa 2022 ilipanda kwa **4.27.**

(v) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2022 yameimarika kwa alama **0.02** kutoka alama wastani **31.19** mwaka 2021 hadi **31.21** mwaka huu. Hali kadhalika, idadi ya watahiniwa waliopata alama za juu imeimarika. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **80/80.** mtahiniwa **1** ndiye



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

aliyepata alama hii. Hali kadhalika, idadi ya wanafunzi waliopata asilimia **70 (56/80)** ilishuka kutoka **10,372** mwaka 2021 hadi **10,199** mwaka 2022. Hali hii inadhihirisha kwamba umilisi wa asilimia kubwa ya wanafunzi katika uchanganuzi wa kufasihi bado ni hafifu mno. Kwa mfano, mwaka huu, alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(17,486) ni 01/80**. Idadi hii imeshuka kutoka **39,330** walioripotiwa mwaka 2021. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi hawa walipata sufuri katika kila swali. Aidha, watahiniwa **58,843** walipata baina ya alama **1/80** na **5/80** katika karatasi hii ikilinganishwa na **95,002** waliokuwa katika kiwango hiki mwaka wa 2021. Hili linadokeza, ama ukosefu wa uhakiki wa makini wa tanzu za fasihi, au unyonge wa wanafunzi katika kusoma vitabu viteule vya Fasihi.

(vi) Licha ya mjadala wa hapo juu, uchanganuzi umeonyesha kwamba alama wastani ya somo la Kiswahili kwa jumla imepanda kiasi kwa alama **4.55** kutoka **82.09** ya mwaka 2021 hadi **86.64** mwaka huu. Hili limetokana na kuimarika kwa alama wastani ya karatasi zote tatu.

(vii) Kadhalika asilimia ya watahiniwa wanaopata gredi A na A- ilipanda, japo haijafikia kiwango cha kuridhisha.

(viii) Hata hivyo ikumbukwe kwamba alama wastani ya somo hili bado haijafikia kiwango cha kuridhisha cha (**100/200**).

### 3.2.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

#### 3.2.2.1 Insha (102/1)

***Jedwali 12: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2014 – 2022***

| Mwaka | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 20.17 | 20.86 | 18.23 | 18.84 | 16.98 | 19.88 | 20.19 | 19.44 | 19.70 |
| Alama ya Tenganisho | 5.26 | 5.19 | 5.53 | 5.23 | 4.82 | 5.43 | 5.28 | 6.28 | 5.69 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba, kwa kipindi cha miaka mitano (2018-2022), utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umekuwa ukiyumba. Tathmini ya kazi halisi za watahiniwa imebainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haimudu kujieleza kwa lugha iliyokomaa. Ni wazi kwamba idadi kubwa ya watahiniwa haikuweza kukuza mada inavyostahili. Aidha, asilimia kubwa ya watahiniwa ilipata chini ya nusu ya alama zilizotengewa karatasi hii **(1/40- 19/40)**. Tathmini ya kazi za watahiniwa pia imedhihirisha kwamba watahiniwa hawamudu maswali yanayoshughulikia masuala yanayowahusu moja kwa moja. Mgao mkubwa wa watahiniwa haukuweza kufafanua, kwa mfano, namna ya kuboresha hali ya wanafunzi wenzao shuleni (Swali la Kwanza). Wengine walishindwa kufafanua manufaa ya Riadha (Swali la Pili). Kuna baadhi ya watahiniwa ambao hawakufahamu dhana ya Riadha. Watahiniwa hao walichukulia Riadha kuwa jina la mtu. Hii ni ishara kwamba wanafunzi wengi, ama wamekosa ubunifu, au hawana mazoea ya kusoma kwa kina na kwa mapana. Kadhalika imebainika kwamba bado swali linalohusu methali halivutii idadi kubwa ya wanafunzi. Idadi ya watahiniwa walioteua swali lililorejelea methali ilikuwa ndogo ikilinganishwa na maswali mengine. Hata hivyo, walioliteua swali hili walimudu kubuni kisa kinachoafikiana na maana ya methali hii, licha ya kiwango chao cha chini cha ubunifu.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**Lazima**

Fadhila ni miongoni mwa wanafunzi wanaogombea nafasi ya kiranja mkuu katika shule ya upili ya Kumekucha. Hekima anamhoji kuhusu mikakati atakayoweka ili kuboresha hali ya maisha shuleni. Andika mahojiano hayo.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika mahojiano baina ya wahusika Fadhila na Hekima kuhusu namna ya kuboresha hali ya maisha shuleni.

Tungo za watahiniwa zilidhihirisha kiwango cha chini cha ubunifu. Wengi hawakuweza kukuza mada kikamilifu. Baadhi hawakuweza kuandika kwa mtindo wa mahojiano. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawatilii maanani usomaji wa mapana, hivyo hawadiriki kushughulikia masuala mtambuko ipasavyo katika tungo zao.

**Ushauri kwa walimu**

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, Kenya (KICD).

**Mapendekezo**

(i) Walimu waendelee kuwashirikisha wanafunzi katika mazoezi zaidi katika uandishi wa kazi za kiuamilifu na tungo za kiubunifu.

(ii) Walimu watilie maanani matumizi ya silabasi ya KICD ili kuelekeza ufundishaji wao. Nyenzo nyinginezo kama vile mwongozo unaotolewa na Baraza la Mitihani kuhusu mada na stadi zinazotahiniwa, pamoja na vitabu vya Fasihi vinavyotahiniwa, zitumiwe kujalizana na silabasi ya KICD.

(iii) Wanafunzi wahamasishwe kuhusu manufaa ya kuboresha stadi ya kusoma, hasa kusoma kwa mapana, na kwa kina. Kusoma huku kutapalilia ubunifu wao. Pia kutawawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala ibuka na mtambuko iwapo yatatahiniwa.

(iv) Walimu wateue novela nyepesi/ vitabu vya hadithi kuanzia kidato cha kwanza na kuhakikisha kuna kipindi cha kusoma kwa sauti na kwa kina ili wanafunzi wakuze stadi za usomaji. Wanafunzi wahimizwe kusoma novela hizi nje ya darasa ili kujifunza kutokana na mitindo anuwai ya kujieleza katukoa kwenye novela, vitabu vya hadithi au matini nyingine.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

### 3.2.2.2 Lugha (102/2)

**Jedwali 13**: ***Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2014 hadi 2022***

| Mwaka | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 32.27 | 36.12 | 34.11 | 25.45 | 27.22 | 36.50 | 34.99 | 31.46 | 35.73 |
| Alama ya Tenganisho | 12.60 | 13.50 | 13.83 | 13.42 | 10.88 | 12.64 | 12.81 | 12.93 | 12.45 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameimarika kutoka **31.46** mwaka 2021 hadi **35.73** mwaka huu.

Swali la kwanza liliwatatiza sana watahiniwa wengi. Swali hili liliwahitaji watahiniwa kusoma kifungu cha ufahamu kisha kujibu maswali. Asilimia kubwa sana ya watahiniwa haikumudu maswali yaliyowahitaji kutumia ujuzi wao kupata majibu. Haya ni maswali yanayolenga kukuza stadi za ufasiri na tathmini au kiwango cha juu cha utambuzi kama vile uchanganuzi, usanisi na tathmini.

Swali la Pili nalo liliwahitaji watahiniwa kusoma kifungu kisha kutoa Muhtasari wa kifungu hicho kwa kurejelea masuala mbalimbali katika kifungu kwa mujibu wa maswali yaliyoulizwa. Kazi husika za wanafunzi zilidhihirisha upungufu katika stadi za kubaini masuala muhimu katika matini na kuandika muhtasari. Baadhi ya watahiniwa hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo; walinakili yale yaliyokuwa katika kifungu, na kuishia kupoteza alama kwa kuzidisha idadi ya maneno. Wengine walifupisha na hata kukosa kujumuisha hoja zote muhimu zilizohitajika. Hivyo, kukosa alama kwa kuwa hawakujadili hoja zote zilizohitajika.

Kadhalika, tathmini ya majibu ya watahiniwa katika Swali la Tatu (Matumizi ya Lugha) ilionyesha umilisi hafifu wa stadi za lugha. Asilimia kubwa mno la watahiniwa haikufikia kiwango kidogo zaidi cha umilisi (kupata majibu sahihi kwa angaa nusu ya maswali katika sehemu hii).

Ruwaza hii ya utendaji pia inadhihirika katika Swali la Nne (Isimujamii) ambalo lilitathmini uwezo wa mwanafunzi kutumia lugha kimuktadha. Swali hili lilitahini sajili ya Viwandani. Wanafunzi wengi hawakumudu kutumia ujuzi wao kung'amua sajili ya Viwandani. Wengi waliiainisha kwa ujumla kama sajili ya Sokoni. Hali kadhalika, japo baadhi ya wanafunzi walitambua sajili ya Viwandani, hawakumudu kulishughulikia swali hili kwa kina kwa kupungukiwa na hoja. Kazi za watahiniwa wengi zilisheheni makosa ya sarufi na hijai ambayo yaliwakosesha alama.

Tutachanganua swali la tatu.


For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**Swali la 3: Matumizi ya Lugha**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika irabu zenye sifa zifuatazo: (alama 1)

(i) mbele, juu, tandazwa ..........................................................................................

(ii) nyuma, kati, viringwa ..........................................................................................

(b) Bainisha silabi inayotiwa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) bingiria ..........................................................................................

(ii) walimwengu ..........................................................................................

(c) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo: (alama 2)

(i) anavyojenga

(ii) mfariji

(d) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mkulima yupo shambani anapalilia mimea.

(e) Andika sentensi ifuatayo katika umoja: (alama 1)

Waashi walijenga majumba ya kifahari ya kupendeza.

(f) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (alama 1)

Wahandisi walikarabati barabara zote baada ya mafuriko.

(Anza kwa: Barabara ...)

(g) Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Serikali imebuni mikakati ya kukabiliana na <u>nzige wengi</u> wanaovamia mashamba.

(h) Alama ya mshazari hutumiwa kutenga nambari. Tunga **sentensi moja** kuonyesha matumizi mengine ya alama ya mshazari. (alama 1)

(i) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 1)

Wanariadha wameenda uwanjani kufanya mazoezi.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(j) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo.

(i) Watalii walifika katika mbuga ya Tsavo walikowaona wanyamapori. (Tumia 'amba') (alama 1)

(ii) Mkurugenzi aliwashauri wafanyakazi wajibidiishe kazini. (alama 2)

(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino)

(k) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Vipepeo wale weupe wanaashiria mvua ya masika inayotarajiwa mwakani.

(l) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Wanakijiji waliwajengea wakongwe nyumba kwa mawe. (alama 3)

(m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)

Huduma za afya zilipoboreshwa, viwango vya maambukizi vilipungua.

(n) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Watunza mazingira watanadhifisha soko letu kesho." Chifu aliwaambia wafanyabiashara.

(o) Tunga **sentensi mbili** kuonyesha **matumizi mawili** ya kiambishi **'-ka-'** (alama 2)

(p) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) bendera ..........................................................................................................

(ii) ujana ..........................................................................................................

(q) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)

Ngoma hizo zimetengenezwa kwa ngozi laini.

(r) Tunga sentensi ukitumia kihisishi kinachoibua hisia za kinyume cha matarajio. (alama 1)

(s) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 3)

$KN(N + \bar{S}) + KT(T) + KN(N + V)$

(t) Bainisha **maana mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Jena angalifuata ushauri wa mwelekezi wake angalifaulu.

(u) Baraste ni kwa barabara, hekima ni kwa ........................ na sihi ni kwa ..........................
(alama 2)



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke

(v) Tunga **sentensi moja** kubainisha **maana mbili** za neno **hema**. (alama 2)

(w) Rafiki yako ana mazoea ya kutoa visababu ili asifanye kazi fulani. Andika methali unayoweza kutumia kumwonya dhidi ya tabia hiyo. (alama 1)

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi. Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi na za matumizi ya lugha kujibu maswali aliyopewa. Imebainika kwamba utendaji wa wanafunzi katika dhana za kimsingi za lugha kama vile ugeuzaji, uakifishaji, aina za maneno, nyakati na hali, kuandika katika umoja na wingi, ukanusho, mnyambuliko wa vitenzi, uchanganuzi wa muundo wa sentensi na uchanganuzi wa maana katika kiwango cha sentensi unaendelea kuwa hafifu. Ni wazi kwamba tatizo hili linachangia kuongezeka kwa makosa ya sarufi, hijai na kimuundo katika mawasiliano. Hili lina athari za kudumu katika utendaji katika sehemu nyingine za karatasi hii.

**Mapendekezo**

1.1.1 Stadi ya kusoma kwa ufahamu ikuzwe kuanzia vidato vya awali. Walimu wawahimize wanafunzi kusoma vitabu vyepesi vya hadithi, novela na makala anuwai ili kujiimarisha katika kuchanganua masuala mbalimbali katika matini. Hivyo, kuboresha stadi za kusoma na kuchanganua matini.

1.1.2 Ufunzaji wa ufahamu uboreshwe kwa kumhusisha mwanafunzi zaidi.

1.1.3 Shughuli za ujifunzaji zizingatiwe zaidi katika ujifunzaji wa stadi na mada za lugha kwa jumla. Walimu wawashirikishe wanafunzi katika tathmini endelevu kupitia mazoezi ya mara kwa mara wakizingatia vipengele vyote vya lugha.

1.1.4 Wanafunzi watathminiwe katika stadi za juu za tambuzi yaani, matumizi, uchanganuzi, usanisi na tathmini. Walimu waandae mazoezi ambato yanayohimiza ukuzaji wa umilisi wa stadi za juu. Walimu wasijikite tu katika maswali na shughuli zinazowafanya wanafunzi kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye muktadha uliotolewa au kukariri kutoka kumbukizi zao.

1.1.5 Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku wakihimizwa kuzingatia mtiririko ufaao ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

1.1.6 Walimu wasisitize vipengele vyote vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

1.1.7 Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe. Mathalan mwalimu anaweza kutumia Fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na masomo mengine hivyo kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.

1.1.8 Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

1.1.9 Masuala yote katika silabasi yazingatiwe.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

### 3.2.2.3 Fasihi (102/3)

**Jedwali 14**: ***Matokeo ya Karatasi ya tatu (102/3) ya miaka 2014 hadi 2022***

| Mwaka | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 42.93 | 38.80 | 25.67 | 25.15 | 22.20 | 21.08 | 25.88 | 31.19 | 31.21 |
| Alama ya Tenganisho | 15.81 | 15.38 | 12.87 | 13.42 | 11.95 | 12.64 | 16.00 | 19.48 | 17.42 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii uliimarika japo kwa kiwango hafifu. Hata hivyo, bado kuna aslimia kubwa (**17,486**) ya watahiniwa ambayo ilipata alama **1/80.** Hali kadhalika, karatasi za watahiniwa zimebainisha kwamba changamoto kuu inayoukumba utendaji wa wanafunzi katika Fasihi ni, ama kutozingatia vipengele muhimu vya uchanganuzi wa kifasihi wanapovisoma vitabu viteule, au kutovisoma vitabu hivyo. Ithibati ya haya ni kutoweza kutambua mhusika katika muktadha uliotolewa, pamoja na kuwachanganya wahusika; mtahiniwa akajadili sifa za mhusika mwingine badala za yule aliyelengwa na swali au akajadili sifa za mhusika badala ya umuhimu. Kadhalika, kazi za watahiniwa zilibainisha kutomudu maswali ambayo yanamhitaji mtahiniwa kujadili umuhimu wa vipengele vya kiploti kama vile mandhari katika kuvijenga vipengele vingine vya kazi husika kama vile wahusika na maudhui. Juu ya hayo, japo baadhi ya watahiniwa walilimudu swali la Fasihi Simulizi, yaelekea kwamba ujifunzaji wa utanzu huu bado ni hafifu. Asilimia kubwa iliepuka swali hili. Baadhi ya waliolifanya hawakumudu kujibu maswali yaliyowahitaji kutumia viwango vya juu vya utambuzi kujibu mwaswali kutokana na utungo waliopewa Watahiniwa hawa hawakumudu kujibu ipasavyo maswali yaliyolenga kukuza stadi za kiwango cha juu cha utambuzi kama vile uchanganuzi, usanisi na tathmini, hasa swali lilitowahitaji kufafanua matatizo ambayo wanaweza kukumbana nayo katika utafiti kuhusu kipera cha Mighani.

Hali kadhalika, tathmini ya karatasi halisi za watahiniwa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa, hata wale wanaopata alama za juu zaidi katika karatasi hii, bado haimudu kuwasilisha hoja kwa njia komavu. Kadhalika, tatizo la kuwasilisha hoja kwa ufupi mno bila kuzitolea mifano na maelezo kutoka matini husika ya kifasihi limeendelea kushuhudiwa. Hili linawafanya watahiniwa wengi kupoteza alama. Vile vile maswali ya ushairi yangali yanaepukwa na idadi kubwa ya watahiniwa. Hata wale wanaodiriki kuyashughulikia, utendaji wao ungali hafifu. Inakisiwa kwamba baadhi ya masuala ya kimsingi ya ushairi kama vile bahari ya shairi na toni hayafunzwi kikamilifu, hivyo yanapotokea katika mtihani watahiniwa wengi hupoteza alama kwa kutoweza kung'amua masuala husika. Hawamudu kutumia ujuzi wa dhana husika kujibia maswali.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

## SEHEMU A: RIWAYA

### A. Matei: *Chozi la Heri*

1. **Lazima**

(a) "... ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba. Elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo wala si fujo na chuki. Mwenzako labda ana hofu kwa vile anaona uhuru wake umeingiliwa. Pengine hata ni mzaha tu..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 6)

(b) Jadili mbinu anazotumia msemaji na wenzake wa jinsia yake katika kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo maishani kwa kurejelea riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 10)

Hili lilikuwa swali la kimuktadha ambalo lilimhitaji mtahiniwa kuwa ameisoma Riwaya ya *Chozi la Heri* kwa kina ili kubainisha matukio katika hadithi na hivyo basi kung'amua wahusika, matendo na sifa zao. Swali hili pia lilihitaji mtahiniwa kufafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo alilodokezewa. Moja kati ya maswali katika sehemu hii lilimhitaji mtahiniwa kujadili mbinu zilizotumiwa na wahusika katika kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo kwa kurejelea Riwaya teule. Asilimia muhimu ya watahiniwa ilishindwa kutambua na kufafanua mbinu hizo na kubakia katika kiwango cha chini cha utendaji. Hili lilidhihirisha umilisi finyu wa stadi za uwazaji kina na uchanganuzi.

Hali kadhalika, uchanganuzi wa utendaji wa watahiniwa katika swali hili, na hata katika maswali mengine ulidhihirisha usomaji hafifu wa vitabu vya fasihi. Watahiniwa wengi hawakuweza kuliweka dondoo katika muktadha. Pia, hawakuweza kutambua mhusika aliyerejelewa. Mbali na hayo, imedhihirika kwamba wanafunzi wengi hawazielewi istilahi za kimsingi za uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walishindwa kuchanganua mtindo katika baadhi ya madondoo. Wengine hawakuelewa dhana za kimsingi za ushairi kama vile bahari ya shairi, kuandika kwa lugha ya kinathari, toni na aina za urudiaji.

### 3.2.2.4 Mapendekezo

(i) Walimu wawaongoze wanafunzi kuvisoma na kuvichambua vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:

a) Dhamira na maudhui
b) Fani, kama vile:
  - Mandhari- Maana na umuhimu wayo;
  - Ploti- vipengele kama vile mbinu rejeshi, elekezi na sadfa, na umuhimu wavyo;
  - Usimulizi- nafsi na wakati katika usimulizi;
  - Wahusika- Sifa na umuhimu wao katika kuzijenga kazi za kifasihi;
  - Muundo- urudiaji, usambamba....,n.k
  - Mtindo, kama vile taswira, kinaya toni, n.k


For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(ii) Wanafunzi wahimizwe kusoma na kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika vitabu viteule.

(iii) Wanafunzi wawekewe misingi bora katika Fasihi Simulizi tangu kidato cha kwanza na kuongozwa kujiimarisha katika mada zote za Fasihi Simulizi kulingana na upeo uliopendekezwa na mtaala wa Shule za Upili.

(iv) Walimu wawaelekeze wanafunzi wao kutambua na kutumia istilahi muhimu za ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya ushairi.

(v) Mbinu za kuchanganua ushairi zifunzwe katika upana na kina kulingana na kiwango hiki.

(vi) Wanafunzi wakumbushwe kwamba vipengele vya kazi ya kifasihi ni vile vile. Kwa mfano; taharuki na toni huweza kuchanganuliwa katika ushairi, na vilevile katika tamthilia na tungo za kinathari, kama vile riwaya.

(vii) Ujifunzaji wenza uhimizwe ili wanafunzi waweze kujifunza kutoka kwa wenzao. Hili linaweza kufanikishwa kwa mwalimu kuwagawa wanafunzi katika vikundi vidogo vitakavyowawezesha kufanya utafiti kuhusu mada mbalimbali na kuwasilishiana ili kujiimarisha.

(viii) Walimu na wanafunzi wafaidike kwa kutumia mitandao na vifaa vya kidijitali kubadilishana mawazo. Walimu wanaweza kuwahimiza wanafunzi kutumia mitandao kwa njia ifaayo kujifunza kutoka kwa wenzao wa shule nyingine. Walimu wanaweza kuwaelekeza wanafunzi kubuni jumuiya ya kimtandao za kujifunzia kupitia, kwa mfano, ukumbi wa *WhatsApp*. Hapo wanaweza kutuma masuala ambayo yanawapa changamoto.

***Tanbihi: Ni muhimu walimu na wanafunzi kukumbuka kwamba mitandao hii haipaswi kuwa vyanzo vya udanganyifu katika mitihani na tathmini mbalimbali. Sharti maadili yadumishwe katika mitandao yote inayotumiwa katika ujifunzaji.***

(ix) Hali kadhalika, ipo haja ya walimu kuandaa warsha na makongamano ili kufanikisha kujadiliwa kwa mada na stadi ambazo zinaelekea kuwatatiza zaidi walimu na wanafunzi.

### 3.2.2.5 Hitimisho

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa jumla umeimarika mwaka huu. Vilevile ni dhahiri kwamba matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa jumla bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha. Inatumainiwa kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa, na kwamba watazingatia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuendelea kuimarisha utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes